Uendeshaji

Benki ya Dunia huepeana fedha kwa riba ya kiasi chachini, bila riba, ama kwa karadha kwa nchi ambazo hazina namna ya kupata mikopo ama ikiwa hazina nanamna njema ya kushughulikiwa katika masoko ya kimataifa

Udhamini **Kukopesha** **Ushauri**

Benki ya Dunia ni mmoja tu kati ya wenye kupeana fedha kwa nchi zinazoendelea; udhaminin wake ni wa asilimia 7 ya utowaji wake wa pesa. Baki ya kiwango hichi—asilimia 93—ina asili ya aina mbalimbali, asili kubwa zaidi ikiwa ni ile ya sekta ya uwekezaji wa kibinafsi, michango ya pamoja na mikopo. Miongo miwili iliyopita, matumizi ya serikali yamepunguka na matumizi ya kibinafsi yameongezeka. Hata hivyo, pesa za sekta ya kibinafsi siyo za kutosha haswa wakati kukiwa na shida za kiuchumi, na pia huwa hazipatikani kwa nchi masikini zaidi.

Udhamini wa Maendeleo

Benki ya Dunia huandaa aina mbalimbali ya udhamini wa miradi yenye lengo la kupunguza umasikini na kuwezesha kufaulu kwa Malengo ya Millennium ya Maendeleo. Hii ni pamoja na mikopo kutoka kwa International Bank of Reconstruction and Development (IBRD) [Benki ya Urekebisho na Maendeleo] pamoja na karadha kupitia International Development Association (IDA) [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo]. Kunapatikana pia namna nyengine za kupeana karadha. *Aina ya udhamini unaofanywa kwa nchi inayo endelea unategemea kiwango cha mahitaji ya nchi yenyewe.*

IBRD- yenye alama za mikopo za AAA inadhaminiwa kupitia kuuzwa kwa World Bank Bonds [Bondi za Benki ya Dunia]. Katika mwaka wa fedha wa 2002, ilifikisha kiwango cha bilioni $23 katika masoko ya fedha. Kinyume na mashirika ya fedha, Benki haifanyi kazi kwa nia ya kuongeza faida yake—inatumia ubora wa alama zake za mikopo ili kupeana kiwango hicho kidogo cha riba kwa wateja wake wa nchi zinazoendelea.

Wanaopata Mikopo Kutika kwa IBRD. Kwa kawaida, kundi hili linahusisha nchi zenye pato la kati. IBRD hupeana mikopo kwa kiwango cha karibu na sawa ya kile cha masoko lakini yenye kukomaa baada ya mda mrefu zaidi kwa nchi zenye pato la chini ya $5,185 kwa kila mwananchi. Wakopeshaji hawa kwa kawaida huwa wana namna ya kupata pesa katika masoko ya fedha ya kibinafsi. Benki huwezesha kupatikana kwa pesa kwa wingi zaidi, kwa kiwango kizuri zaidi na zenye mda mrefu zaidi za kuwa tayari kwa malipo, na kwa namna yenye mvuto zaidi kushinda katika masoko.

> ***Asilimia sabini na tano ya masikini duniani—wanoishi kwa pato la chini ya $1 kwa siku—wanaishi katika nchi zinazopata usaidizi wa mikopo ya IBRD.***

Pesa zinazokopeshwa na serikali ni wajibu zitumiwe kwa mipango hasusa—kwa mfano: kupunguza umasikini, kupeana huduma muhimu, kuhifadhi mazingira, ama kukuza uchumi. Nchi zinazopata mikopo kutoka kwa IBRD zina mda mrefu zaidi wa kulipa kushinda zinapopata mikopo katika benki ya biashara—miaka 15 hadi 20 kukiwa na miaka mitatu hadi mitano kabla kuanza kulipa kiwango cha mwanzo. Katika mwaka wa fedha 2002 IBRD imepeana mikopo ya kiasi cha bilioni $11.5 kwa kusaidia miradi 96 katika nchi 40. Mikopo ya IBRD (na karadha za IDA) kawaida hufwatiliwa na huduma zisizokuwa za mikopo ili kuhakikisha kuwa na matumizi bora ya fedha.
Mikopo ya IDA isiyokuwa na riba ina mda wa malipo kwa miaka 35 hadi 40 pamoja na miaka 10-bila malipo. Ingawa kwa kawaida IDA imepeana mikopo bila riba, inapeana pia karadha kwa wingi zaidi kwa nchi masikini zaidi. Kwa sasa, ili nchi istahili kupata msaada wa IDA ni lazima iwe na Jumla ya Pato la Taifa lisilo zidi $875.
IDA inadhaminiwa na ushirikiano wa wafadhili wanaokutana kila miaka mitatu kuamua kiasi cha rasilimali kinacho hitajika kudahmini miradi ya baadaye ya mikopo ya IDA na kujadili sera za mikopo na umuhimu wake. Katika mwaka wa fedha 2002 IDA ilipeana kiasi cha bilioni $8.1 kudhamini miradi 133 katika nchi 62 zenye pato la chini. Kuongezwa kwa akiba ya IDA ya hivi karibuni itajumlisha bilioni $23 kwa nchi masikini kwa mda wa miaka mitatu kwanzia Julai 1, 2002. Wafadhili pia waliamuwa kuweko pesa zaidi za karadha.

> ***Kuelekea mbele, asilimia 18 hadi 21 ya rasilimali ya IDA itatumika kwa karadha.***

Karadha za IDA ni robo ya udhamini wa Benki. Na kando ya IDA, kiasi kidogo sana cha pato la Benki litoka kwa nchi wanachama. Kati ya fedha za IBRD, asilimia 5 hutokana na michango ya nchi tajiri, inayolipwa wanapojiunga na Benki.

Udhamini wa pamoja husaidia Benki kuendeleza rasilimali zake kwa udahmini wa zaidi, kawaida bila riba, ama kama karadha ili ifaidi nchi inayopata mkopo. Mbinu za udhamini wa pamoja na hazina zinaandaliwa kwa miradi kupitia ushirikiano. Udhamini wa pamoja unamaanisha kuwa fedha zinatayarishwa na washirika rasmi, washirika mbalimbali, mashirika ya kutoa karadha, ama udhamini wa kibinafsi kwa miradi inayodhamniwa na Benki.

> ***Katika mwaka wa fedha 2002 udhamini wa bilioni $19.5 kutoka kwa IBRD na IDA uliongezwa kwa bilioni $4.7 kutoka kwa wadhamini wengine.***

Heavily Indebted Poor Countries (HIPC) Initiative **[Juhudi ya Nchi zenye Madeni Makubwa],** iliyoanzishwa mwaka 1996 na Benki ya Dunia na Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF), ndiyo mpango wa kwanza wa kimataifa wa kushugulikia mzigo wa madeni. Mpango wa Juhudi hii umeondolea nchi nyingi shida ya madeni, na kuweza kusaidia kupatikana kwa pesa za huduma za jamii.

> ***Kufikia Septemba 2002, nchi 26 zilikuwa zimefikia uamuzi wao kupitia juhudi ya HIPC Initiative na zinapokea msaada wa kupunguza maden iwa kiasi cha bilioni $40.***

Jinsi Mkopo Unavyotayarishwa
Benki hupeana aina mbili za mikopo: mikopo ya uwekezaji katika bidhaa, kazi, na huduma ya kusaidia miradi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika sekta aina mbalimbail. Mikopo ya mageuzi hupeana fedha za upesi za kusaidia mageuzi ya sera. Angalia pia: Where the Money Went in 2002 [Kule Pesa ziliko kwenda Mwaka 2002].
Mara tu mwenye kukopa anapo fanya uamuzi juu ya mradi wake na anapo tayarisha azimio la mradi, Benki hukagua ubora yake. Wakati wa mazungumzo ya kupeana mkopo Benki na mwenye kukopa hukubaliana kuhusu lengo la maendeleo, sehemu zake, faida yake, viasheria vya kufaulu kwake, na mpango wa utekelezaji, na mpango wa kupeanwa fedha za mkopo. Benki inapo idhinisha mkopo, mkopo huwa tayari na mwenye kukopa huekeleza mradi ama programu kulingana na maelewano yake na Benki.
Benki husimamia utekelezaji wa kila mkopo na hukagua matokeo yake. Robo tatu ya mikopo inasimamiwa na wakurugenzi wa nchini ambao wako kando na makao makuu ya Benki Washington, D.C. Karibu wafanyakazi asilimia 30 wa Benki wanapatikana katika ofisi 100 za nchi ulimwenguni.
Mikopo yote inasimamiwa na mifumo ya uendeshaji ya Benki ya Dunia, yenye lengo la kuhakisha kwamba shuhuli zinaodaminiwa na Benki ni za maufaa kifedha, kijamii na zisizo haribu mazingira. Sera za usimamizi wa Mali na mbinu zake huongoza matumizi ya fedha za kutimika katika miradi, haswa zile za kupatikana kwa bidhaa na huduma. Sera za Uangalifu zinasaidia kuzuia mikasa ambayo haikutazamiwa kutokea kwa wahusika wakando wa miradi na pia katika mazingira. Maelezo zaidi yanapatikana kuhusu idara ya sheria na Huduma ya Ushauri ya Maendeleo ya Kudumu ya Mazingira na Kijamii ya Benki.
Ili ikubaliwe, miradi yote ya Benki ni sharti ionyeshe kwamba haita dhuru watu ama mazingira. Mbali na Ukaguzi wa Mazingira unaofanywa na miradi yote, Benki ina sera rasmi kuhusu mazingira, wadudu waharibifu, mali za kitamaduni, kuhamishwa kusiko kuwa kwa hiari, watu wa asili, misitu, usalama wa mabwawa, miradi iliyoko katika maji ya kimataifa, pamoja na miradi katika sehemu zenye kugombaniwa. Hizi sera ni nyingi na hutaliwa na kukaguliwa vyema sana. Ukaguzi wa sera uhusisha washauri wa nje. Kwa mfano, sera hizi kwa sasa zinafanyiwa ukaguzi na nakala zake za matayarisho ziko katika Mtandao na maoni yanakubaliwa kupitia mtandao:

- Mikopo ya Marekebisho
- Viwanda vya Utozaji

Wanachama wa Benki wameidhinisha Sera ye Ufahamisho mpya inayoruhusu Benki kutoa kwa watu nyingi za waraka zake, zikiwemo zile za miradi, Muhtasari wa Mwenyekiti wa Majadiliano ya Bodi kuhusu Country Assistance Strategies (CAS) [Sera za Usaidizi wa Mataifa] na Sector Strategy Papers (SSP) [Mkakati wa Mbinu za Sekta].
Huduma za Mipangilio na Ushauri
Ingawa Benki ya Dunia inajulikana vyema zaidi kama mfadhili wa kifedha, kati ya shughuli zake muhimu zaidi ni kupeana huduma ya mipangilio na ushauri ili kuimarisha mabadiliko ya sera za kudumu.
Mshikano wa Benki wa Uchumi wa Maendeleo, ukiongozwa na mtaalamu wake mkuu wa uchumi, hufanya utafiti unaofahamisha kuhusu kazi za Benki katika mambo mbalimbali kama vile mazingira, umasikini, biashara na utandawazi.
Katika kila nchi wafanyakazi wa Benki wanfanya utafiti wa kiuchumi ambao ndio msingi wa mipango ya nchi hizo. Hii economic and sector work (ESW) [kiuchumi na sekta ya kazi] huangalia makadirio ya kiuchumi, ikiwemo kwa mfano:sekta zake za benki ama fedha, biashara, umasikini, pamoja na maswala ya usalama katika jamii. Utafiti wa Benki unapatikana:

- Utafiti wa Umasikini
- Maelezo ya Matumizi ya Pesa za Umma
- Stakabadhi za Uchumi wa Nchi
- Maelezo ya Kijamii na Uundaji
- Ripoti za Sekta
- Kugawiana Utaalamu

Kuimarisha Uwezo
Kuimarisha uwezo wa kustawisha mipango ya kupunguza umasikini katika nchi ni kazi ya muhimu sana ya Benki ya Dunia. Kuongeza kiasi cha rasilimali kuna nia ya kufanikisha juhudi kazi hii kwa sababu imeonyesha kuweko kwa mafanikio mema. Inajulikana kama Kugawiana Utaalamu, na bidii nyingi ni kupitia World Bank Institute (WBI) [Taasisi ya Benki ya Dunia], inayoendesha programu za kuimarisha ujuzi na maendeleo ya wateja wake, wafanyikazi, na washirika wake. Haya hayafanyiki kwa kutumia masomo tu bali huwa pia na mashauri, ushirika na taasisi za mafunzo na utafiti ulimwenguni, na kuanzisha na kustawisha mishiko ya maendeleo ya kimataifa. WBI ndipo penye makao ya miradi ya masomo ya mbali iliyosambaa sana ulimwenguni. Huduma za Ushauri zinapatikana kwa maelzo na ujuzi uliopangwa kwa mada—iwe ni maendeleo yaliyostawi ya kimanzingira ama kijamii, afya, lisho bora, ongezeko la watu, sekta ya fedha, ama sheria na haki. Wakati mwengine vifaa hupatikana kwa matumizi ya wataalamu wengine wa maendeleo-kwa mfano: upangaji wa miradi; usimamizi na ukaguzi; mahitaji ya kifedha, kisheria, na ya vita vinavyouziwa; maswala ya kijinsia; chakula na lisho bora; pamoja na hakikisho la makao mapya.